JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

MWONGOZO WA USIMAMIZI SHIRIKISHI UNAOHUSISHA JAMII YA WAVUVI WA PWANI YA BAHARI YA HINDI

IMEANDALIWA NA
IDARA YA UVUVI NA SHIRIKA LA WWF

MACHI 2009

WWF
for a living planet®

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

IMEANDALIWA NA
IDARA YA UVUVI NA SHIRIKA LA WWF

MWONGOZO KWA AJILI YA USIMAMIZI SHIRIKISHI UNAOHUSISHA JAMII YA WAVUVI KWENYE PWANI YA BAHARI YA HINDI

WWF *for a living planet*®

MACHI 2009

Kimetolewa na:

Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi,
Idara ya Maendeleo ya Uvuvi
S. L. P. 9152,
Dar es Salaam,
Barua elektroni: ps_ld@mifugo.go.tz

na

Ofisi ya Programu ya WWF Tanzania,
S. L. P. 63117,
Dar es Salaam,
Barua elektroni: JMwangamilo@wwftz.org

© D.A.S. Mbilinyi, A. Masanja. A. Sakara na B. Mahundi, 2007.

ISBN 978-9987-508-03-7

Usanifu: PENplus Ltd - 022 2182059

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi ama kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki.

YALIYOMO

		Uk
Dibaji		iv
Shukrani		vi
Vifupisho		vii
Utangulizi		viii
1.	Sera na Sheria ya Uvuvi	1
2	Usimamizi wa shughuli za uvuvi	5
3	Usimamizi shirikishi wa uvuvi katika Bahari ya Hindi	12
4	Uongozi na Utawala bora	34
5	Jinsi ya kutatua, kuzuia na kuhimili migogoro	39
6	Viashiria kwa ajili ya usimamizi shirikishi kwenye raslimali za pwani na bahari	43
Kiambatanisho Namba 1		46
Kiambatanisho Namba 2		47
Kiambatanisho Namba 3		48
Kiambatanisho Namba 4		49
Kiambatanisho Namba 5		50
Kiambatanisho Namba 6		51
Kiambatanisho Namba 7		52
Rejea		53

DIBAJI

Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kupitia Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani (MACEMP) na Shirika la "World Wide Fund for Nature (WWF)" Ofisi ya Tanzania kwa pamoja zinatekeleza shughuli mbalimbali za hifadhi ya raslimali za pwani na Bahari ya Hindi kwa ajili ya kupunguza umasikini na kuwaletea maendeleo jamii ya wananchi wa ukanda wa pwani ya Bahari ya Hindi. Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani unatekelezwa katika Halmashauri kumi na sita za mwambao wa pwani ya Bahari ya Hindi. Halmashauri hizo ni Pangani, Mkinga, Muheza na Tanga (Mkoa wa Tanga); Bagamoyo, Mafia, Mkuranga na Rufiji (Mkoa wa Pwani); Ilala, Kinondoni na Temeke (Mkoa wa Dar-es -salaam); Kilwa, Lindi Mjini, Lindi (Mkoa wa Lindi) na Mtwara Mikindani na Mtwara (Mkoa wa Mtwara) . Pia, Shirika la WWF kupitia programu ya RUMAKI, linatekeleza miradi ya kuboresha uchumi wa jamii na matumizi endelevu ya raslimali za pwani na bahari katika Wilaya za Rufiji , Mafia na Kilwa.

Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (Idara za Uvuvi), inashirikiana na Wizara za Maliasili na Utalii (Idara ya Misitu na Nyuki), Ofisi ya Makamu wa Rais (Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Halmashauri zote zilizopo katika pwani ya Bahari ya Hindi) na Shirika la WWF katika kuishirikisha jamii ya wananchi kwenye usimamizi shirikishi na matumizi endelevu ya raslimali zao mbazo ni pamoja na samaki, matumbawe na miti ya aina mbalimbali, ardhi na fukwe za bahari.

Ili kufanikisha kazi za usimamizi shirikishi, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani kwa kushirikiana na Shirika la WWF umeandaa mwongozo wa kuziwezesha jamii za pwani ya Bahari ya Hindi kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi (Beach Management Units - BMUs).

Mwongozo huu unaelezea hatua kwa hatua kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Sera na Sheria ya Uvuvi; Usimamizi wa shughuli za uvuvi na Ushirikishwaji jamii katika kusimamia raslimali za pwani na bahari; Utawala bora na Utatuzi wa migogoro pamoja na Viashiria vya kupima kazi za vikundi. Mwongozo huu umeandaliwa ili utumike katika kazi za kuazisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za pwani na Bahari ya Hindi pamoja na sehemu nyingine za uvuvi nchini.

C. Nyamrunda
Katibu Mkuu
Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
Machi 2009

SHUKRANI

Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani (MACEMP) na Shirika la "World Wide Fund for Nature (WWF)" wanatoa shukrani zao za dhati kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la WWF Ofisi ya Tanzania. Wengine ni watu wote ambao kwa njia moja au nyingine walichangia katika utayarishaji wa mwongozo huu. Maoni na ushauri waliotoa katika kuandika mwongozo huu unathaminiwa.

Mwisho, lakini pia ni muhimu, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani na Shirika la WWF wanapenda kuwashukuru watayarishaji wa mwongozo huu ambao ni Bw. Rashid B. Hoza, Afisa Uvuvi Mkuu na Bibi Fatma Sobo, Afisa Uvuvi Mkuu (Idara ya Uvuvi) na Bibi Modesta Medard (WWF). Ushirikiano wao umewezesha kuandikwa kwa mwongozo huu. Pia, shukrani za dhati ziwaendee Bibi Julitha Mwangamilo (Mratibu wa Kitengo cha Usimamizi Shirikishi) na Bw. Ali Thani (Mratibu wa Mawasiliano na Uhamasishaji) wote kutoka Shirika la WWF kwa mchango wao wakati wa kuboresha mwongozo huu.

Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani
Shirika la WWF
Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
Machi 2009

VIFUPISHO

BMU - Beach Management Unit - Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi katika ngazi ya kijiji

BMUs - Beach Management Units - Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi katika ngazi ya kijiji

CFMAs - Collaborative Fisheries Management Areas- Maeneo ya mavuvi ya pamoja

EC - Executive Committee- Kamati Tendaji za Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali ya uvuvi

MACEMP - Marine and Coastal Environment Management Project- Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani

NEMC – National Environmental Managemnt Council - Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira

SACCOS - Savings and Credit Cooperative Society- Chama cha Ushirika wa Kuweka na Kukopa

WDC - Ward Development Committee- Kamati ya Maendeleo ya Kata

WEO - Ward Executive Officer- Afisa Mtendaji wa Kata

WWF - World Wide Fund for Nature

VEO - Village Executive Officer –Afisa Mtendaji wa Kijiji

UTANGULIZI

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya kuanzisha usimamizi shirikishi wa raslimali za pwani na bahari unaohusisha jamii. Kitabu hiki kimeandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha waraghabishi na baadae kitumike kutoa mafunzo kwa jamii.

Mwongozo huu umegawanyika katika masomo sita ambayo ni Sera na Sheria ya Uvuvi; Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi; Usimamizi shirikishi unaohusisha jamii; Utawala bora; Utatuzi wa migogoro na Viashiria.

Wakati wa kutoa mafunzo kwa waragabishi ni lazima kufundisha masomo yote sita ili wafahamu maeneo ya msingi. Baada ya mafunzo wahitimu watawaelimisha jamii ya wavuvi ili waanzishe usimamizi shirikishi wa raslimali za pwani na bahari unaohusisha jamii katika vijiji vyao. Pia, wahitimu (waraghabishi) watatakiwa kutumia elimu waliyoipata kuwafundisha Viongozi wa Serikali za Vijiji, Maafisa Watendaji wa Vijiji, Maafisa Watendaji wa Kata na viongozi wengine wa ngazi za Tarafa na Wilaya.

SURA YA KWANZA:

SERA NA SHERIA YA UVUVI

Tamko la Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake

Sera ya Uvuvi inatoa mwongozo wa mabadiliko ya mwelekeo/tabia katika kushughulikia masuala ya uvuvi pamoja na umuhimu wa usimamizi, kutunza na kuendeleza masuala hayo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo pamoja na kuhakikisha kuwa kunakuwepo na mafanikio/ufanisi. Chombo kinachotumika katika kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uvuvi ni Sheria ya Uvuvi. Sera ya Uvuvi ni chombo cha usimamizi ambacho kina himiza uvunaji, matumizi na biashara endelevu ya raslimali za uvuvi kwa ajili ya kuwapatia wananchi chakula, kipato, ajira na fedha za kigeni na ulinzi thabiti wa viumbe hai wa majini na mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu. Lengo kuu la Sera ya Taifa ya Uvuvi ni kukuza uhifadhi, maendeleo na usimamizi endelevu wa raslimali za uvuvi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Sheria na Kanuni za Uvuvi

Dhumuni la Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 ni kuleta maendeleo endelevu, kulinda, kuhifadhi, kuendeleza ufugaji wa viumbe hai kwenye maji, kudhibiti ubora wa samaki na mazao yake, mimea ya majini na mazao yake na masuala mengine yanayofanana na hayo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Sheria ya Uvuvi juu ya usimamizi shirikishi Sehemu ya Tano (V) ya Sheira ya Uvuvi iitwayo Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Uvuvi. Kifungu cha 18 cha Sheria ya Uvuvi kinaruhusu Serikali ya Kijiji kuanzisha Vikundi vya Usimamizi shirikishi wa raslimali za uvuvi.

Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005 juu ya usimamizi shirikishi
Kanuni ya 104 inahusu usimamizi shirikishi. Pia, Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005 zimefanyiwa marekebisho ya kuboresha Kanuni za Uvuvi kuhusu usimamizi shirikishi unaohusisha jamii. Marekebisho hayo yatakapo idhinishwa na Waziri mwenye dhamana ya kusimamia masula ya uvuvi yatasaidia kuimarisha Sheria na Kanuni za Uvuvi juu ya usimamizi shirikishi unaohusisha jamii katika kuongeza ufanisi kwenye kutekeleza majukumu ya vikundi vya usimamizi wa raslimali za uvuvi. Usimamiaji wa Sheria ya Uvuvi unaimarisha maendeleo, kulinda, kuhifadhi, kuendeleza, kusimamia, kuvuna, kutumia na kuuza samaki na mazao yake kwa njia endelevu kwa lengo la kuwapatia wadau chakula, uchumi, ajira na fedha za kigeni na kuwa na ulinzi timilifu wa viumbe wa baharini na mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Matatizo yaliyopo kwenye kutekeleza Sera ya Uvuvi na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Uvuvi

- Sera mtambuka zinazohusiana na kulinda, kuendeleza, kusimamia na kutumia raslimali ikiwa ni pamoja na zile za uvuvi bado hazijaainishwa/zinatofautiana
- Serikali haina fedha za kutosheleza mahitaji ya kuiendeleza sekta (watumishi, vitendea kazi na fedha)
- Hakuna udhibiti wa kutosha wa idadi ya nyavu, wavuvi na mitumbwi kwenye ukanda wa pwani, bahari, maziwa, mabwawa na mito
- Utaratibu wa kiutawala wa kusimamia masula ya uvuvi kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu una mapungufu mengi
- Hakuna juhudi za kutosha za kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na samaki katika kuongeza kipato cha wadau na Serikali

- Mfumo wa kukusanya, kuandaa na kutunza takwimu hautoshelezi
- Takwimu zilizopo haziaminiki na mfumo wa usamabazaji takwimu na taarifa za uvuvi sio thabiti

Fursa zilizopo kwenye Sera ya Uvuvi na Sheria ya Uvuvi

- Siasa iliyopo inahimiza matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi
- Kuwepo kwa raslimali ya uvuvi katika bahari na pwani (Bahari ya Hindi), maziwa, mabwawa na mito
- Kuwepo kwa wadau wanaojihusisha na uvuvi endelevu
- Kuwepo kwa wahisani, sekta binafsi, Mashirika yasiyo ya kiserikali na wengine ambao wanasadia juhudi za Serikali katika kutunza na kuendeleza raslimali za uvuvi kwa njia endelevu
- Kuwepo kwa Sera na Sheria ya Uvuvi
- Kuwepo kwa Taasisi za Serikali zinazosaidia katika kutunza na kuendeleza raslimali kwa njia endelevu
- Kuwepo kwa wadau ambao wamepewa mamlaka kisheria ya kusimamia Sheria ya Uvuvi

Matatizo ya kusimamia Sheria ya Uvuvi

- Kuwepo kwa uvuvi haramu na umasikini kwenye jamii ya wavuvi
- Upungufu wa watumishi na fedha za kudhibiti idadi ya wavuvi, mitumbwi na nyavu/mitego
- Ufanisi mdogo katika kusimamia Sheria na Kanuni za Uvuvi
- Uhaba wa shughuli ndogo ndogo za kuwapatia ajira na uchumi mbadala wananchi wa maeneo ya pwani
- Ushirikiano hafifu baina ya Idara ya Uvuvi, Serikali za Mitaa na Polisi na Mahakama katika kusimamia Sheria na

Kanuni za Uvuvi

- Kutofautiana katika maoni na maslahi kwenye sekta ya uvuvi kati ya wadau na taasisi zingine

Baadhi ya changamoto zilizoko kwenye Sera na Sheria ya Uvuvi

- Kuendelea kulinda, kuendeleza, kusimamia na kutumia raslimali za uvuvi kwa njia ya kujitegemea ambayo ni endelevu na kupata msaada kidogo kutoka kwa wafadhili
- Kuimarisha ushirikiano baina ya wadau ili kuleta maendeleo, kulinda, kuhifadhi, kuendeleza, kusimamia, kuvuna na kutumia raslimali za uvuvi kwa njia endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo
- Kuanzisha mfumo thabiti wa kudhibiti uvuvi haramu, idadi ya wavuvi, mitumbwi na mitego na kutambua na kuendeleza kazi na uchumi mbadala wa wakazi wa pwani
- Kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa Idara ya Uvuvi na jamii ya wavuvi kuhusu kulinda, kutunza na usimamzi wa raslimali za uvuvi, ujasiriamali, ongozi na utawala bora, kutatua migogoro ya wadau, ushirika nk
- Kuimarisha usimamizi shirikishi wa raslimali za pwani na bahari unaohusisha jamii
- Kupitia na kufanya marekebisho ya mara kwa mara ya Sera na Sheria ya Uvuvi

SURA YA PILI:

USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI

Ni mwingiliano wa mchakato wa mkusanyiko wa ukusanyaji na uchambuzi wa habari za uvuvi, mipango ya uvuvi, kusimamia shughuli zote zihusuzo uvuvi pamoja na maamuzi mbali mbali ya uvuvi. Hii ni pamoja na ushirikishwaji katika utungaji na utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Uvuvi. Yote haya yana umuhimu katika uvuvi endelevu na kukidhi au kutimiza malengo yaliyopangwa. Usimamizi wa uvuvi ni utaratibu mzima wa kazi na mipango ya maswala ya uvuvi yenye lengo la kuhakikisha kwamba faida ya uvuvi inapatikana kwa watumiaji wa uvuvi, serikali na kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mazao ya uvuvi unadumu kwa faida ya watumiaji.

Umuhimu wa usimamizi wa uvuvi

- Kuweka sera na maazimio kwa kila aina ya uvuvi au usimamizi wa uvuvi huo, kwa kuzingatia bioanuwai ya uvuvi huo, kuwepo kwa aina hiyo ya uvuvi au upatikanaji wa uvuvi huo kwa muda mrefu pamoja na yale yanayoendana na maswala ya uvuvi.
- Kufuatilia na kuweka nguvu, kuwezesha uongozi na usimamizi, wavuvi na vikundi vingine, kufanya kazi kwenye mipango inayokubalika.
- Kukubaliana na kutekeleza yale yote ambayo ni muhimu katika usimamizi kwa watumiaji au vikundi juu ya madhumini yaliyopangwa.
- Kuhusisha na kukubaliana na watumiaji na makundi yote yanayohusika na uvuvi kuhusiana na namna ya kuingia katika uvuvi.
- Kuweka utaratibu wa kupitia kwa njia ya kuwashirikisha

wadau madhumini, mipango na mikakati kila baada ya muda ili kuhakikisha kwamba yote yaliyopangwa bado yanaumuhimu unaotakiwa.
- Kuwasilisha kwa serikali, watumiaji na wananchi wote kwa ujumla taarifa ya raslimali za uvuvi iliyopo.

Uvuvi endelevu, usimamizi, uhifadhi, maendeleo na matumizi ya raslimali za uvuvi

Ni matumizi ya uvuvi yanayo hakikisha kwamba uvuvi unaendelea kufanyika kwenye maeneo ya uvuvi bila kuathiri mayai, samaki wachanga, samaki wazazi na maeneo wanamo ishi ili jamii liendelee kuvuna bila ya kumaliza raslimali za uvuvi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Matatizo, fursa na changamoto katika usimamizi wa uvuvi

- Upungufu wa wataalamu na fedha katika maswala yote yahusuyo ukusanyaji wa takwimu na taarifa za uvuvi, kuanzia namna ya kuzikusanya, kuzichanganua na jinsi ya kuzisambaza kwa watumiaji.
- Mipango ya sekta ya uvuvi inapangwa sana katika ngazi za juu matokeo yake ni kwamba kuna ushirikishwaji mdogo wa jamii ya wavuvi hasa ngazi ya kijiji.
- Udhaifu katika maswala ya usimamizi wa Sheria na Kanuni za Uvuvi.

Fursa katika sekta ya uvuvi

- Kuwepo kwa Sera ya Taifa ya Uvuvi, Sheria na Kanuni za Uvuvi kunaimarisha uvuvi endelevu, usimamizi na matumizi endelevu ya mazao yatokanayo na uvuvi
- Kuwepo kwa Idara za Serikali, Tasisi za Serikali, wadau binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi kwa ujumla wanaosisitiza matumizi endelevu ya uvuvi, uhifadhi,

maendeleo ya uvuvi pamoja na matumizi endelevu ya samaki na mazao ya uvuvi.

- Siasa inayokubalika na ambayo inakubali uvuvi endelevu, maendeleo ya uvuvi na matumizi sahihi ya samaki na mazao ya uvuvi.
- Kuwepo kwa vyuo vya mafunzo ndani na nje ya nchi vinavyotoa Shahada, Stashahada, Astashahada nk za utaalamu na ufundi katika maswala ya uvuvi hasa uvuvi endelevu, uhifadhi wa samaki na mazao yake, maendeleo na matumizi sahihi ya samaki na mazao ya uvuvi.
- Upatikanaji wa shughuli mbadala ili kupunguza uvunaji wa raslimali za uvuvi katika kuhakikisha kuwa raslimali iliyopo inaendelezwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.
- Lugha ya Kiswahili kuongelewa na Wa-Tanzania wote imechangia katika kuongeza fursa kwenye sekta ya uvuvi kwa maana ya kuleta umoja wa kitaifa katika kutekeleza Sera ya Uvuvi
- Kuwepo kwa uwazi katika kujadili masuala mbali mbali na hivyo kuleta changamoto kwa watendaji na wadau mbalimbali

Changamoto katika Usimamizi wa Uvuvi

- Kuimarisha mchakato mzima wa ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu, taarifa za uvuvi, na kusambaza taarifa hizo kwa wakati ili kuweka mipango thabiti, maendeleo na usimamizi mzuri
- Kutengeneza mkakati mbao utahakikisha kuwa wadau wa uvuvi wanashauriwa na kuhusishwa katika kila mpango unaotaka kuanzishwa au kuendelezwa
- Kuendelea kutoa utaalam kwa watumishi wa Idara ya Uvuvi, Serikali za Mitaa, wavuvi, wachuuzi, wachakataji,

wasuka nyavu na wananchi kwa ujumla juu ya maswala yote yahusuyo uvuvi endelevu na usimamizi wake
- Kushirikisha na kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia shughuli za uvuvi
- Kuimarisha ushirikiano wa kisekta katika kufanya kazi kwa pamoja kwenye maswala ya utafiti na usimamizi wa uvuvi

Majukumu ya usimamizi wa uvuvi kwa wadau

Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi (Beach Management Units- BMUs) katika ngazi ya Kijiji
- Kusimamia Sheria na Kanuni za Uvuvi
- Kutayarisha Sheria ndogo ndogo zitakazosaidia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Uvuvi
- Kuhakikisha kwamba mwalo ni safi na unafaa kutumika
- Kukusanya takwimu
- Kutoa mafunzo kwa wadau kuhusu madhara ya matumizi ya zana haribifu pamoja na maswala yote ya uharibifu wa mazingira unaochangia katika uharibifu wa raslimali za uvuvi
- Kutayarisha na kutekeleza miradi ya maendeleo
- Kusimamia usalama wa watu na mali zao
- Pamoja na kazi zingine zifaazo kutekelezwa na BMU

Serikali za Vijiji

Majukumu ya Serikali ya kijiji ni pamoja na:
- Kupitisha Sheria ndogo ndogo zilizoletwa na vikundi vya usimamizi wa raslimali za uvuvi na mazingira
- Kupokea Sheria ndogo ndogo za vikundi vya usimamizi wa raslimali za uvuvi, na kuziwasilisha kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata (Ward Development Committee - WDC) ili zipitishwe na kuwasilishwa "Full Council" ya

Halmashauri ya Wilaya

- Kusaidia vikundi vya usimamizi wa raslimali za uvuvi katika kazi zao za kila siku za usimamizi wa raslimali za uvuvi na mazingira
- Kusaidia vikundi vya usimamizi wa raslimali za uvuvi katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo ndogo ili kuboresha utekelezaji wa Sheria mama zinazohusiana na utunzaji na matumizi endelevu ya raslimali za bahari na pwani

Halmashauri za Wilaya

Kazi zifuatazo zinatekelezwa katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya:

a) Kusimamia Sheria na Kanuni za Uvuvi
b) Kupitisha Sheria ndogo ndogo za vikundi vya usimamizi wa raslimali za uvuvi na mazingira zilizowasilishwa na WDC
c) Kutoa elimu ya ugani
d) Kufuatilia ukusanyaji wa takwimu za uvuvi
e) Kutoa msaada wa kitaalam kwa wadau hasa kwa wale ambao ni watendaji wa miradi ya uvuvi
f) Kutayarisha mipango ya muda mfupi na mrefu ya sekta ya uvuvi
g) Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya Wilaya
h) Kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za uvuvi na kuyagawa ipasavyo

Idara ya Uvuvi katika ngazi ya Taifa

Idara ya uvuvi ndiye msimamizi mkuu wa Sheria na Kanuni za Uvuvi na inatoa mwongozo na usimamizi wa raslimali ya uvuvi kwa kupitia Sera ya Uvuvi. Kazi nyingine ni

a) Kutayarisha na kuboresha Sera, Sheria na Kanuni za Uvuvi

b) Kutayarisha mipango ya muda mfupi na mrefu ya maendeleo ya uvuvi
c) Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya uvuvi
d) Kusimamia Sheria na Kanuni za Uvuvi
e) Kutoa mafunzo kwa watumishi na wadau wengine kwenye mambo yahusuyo utunzaji, hifadhi, maendeleo na matumizi endelevu na usimamizi wa raslimali ya uvuvi. Mafunzo mengine ni uzuiaji uharibifu wa samaki na mazao ya uvuvi na kukusanya mapato yatokanayo na uvuvi, ushirika na ujasiriamali, kutayarisha Sheria ndogo ndogo, mafunzo ya usimamizi wa fedha na uongozi,
f) Kuimarisha ushirikiano na maelewano na wadau
g) Kukusanya takwimu na habari zote za uvuvi
h) Upashanaji habari kwa wadau
i) Kusaidia shughuli za ugani

Mashirika yasiyo ya kiserikali na yale ya kijamii

Mashirika yasiyo ya kiserikali na yale ya jamii yanaweza kusaidia na kuimarisha na kujenga vikundi vya usimamizi wa raslimali za uvuvi kwa kuwapatia mafunzo na utaalam mwingine unaohusika na hayo, ili kukuza/kulinda raslimali ya uvuvi, uhifadhi na kukuza uvuvi endelevu na matumizi sahihi ya raslimali za uvuvi. Kwa hiyo kazi za mashirika yasiyo ya kiserikali na yale ya jamii ni pamoja na:

a) Kukuza uelewa na kuboresha shughuli za ugani
b) Kutoa mafunzo na utaalaam wa swala linalohusika
c) Kuwapatia uwezo wa kifedha vikundi vya usimamizi wa raslimali za uvuvi katika shughuli zihusuzo mazingira, uhifadhi na usimamizi endelevu wa raslimali za uvuvi
d) Kukuza maswala ya jinsia na kuwapa kipaumbele wadau au watumiaji wa raslimali za uvuvi
e) Kushirikiana kwa dhati na vikundi vya kusimamia

mazingira katika maeneo yao

Mashirika na Taasisi za watu binafsi

Mashirika ya watu binafsi nao wana kazi ya kukuza maendeleo ya uvuvi. Uwekezaji wao ni chanzo tosha cha ajira, kuongezeka kwa biashara na mchango wao katika kulipa kodi/ushuru. Mchango wao unasaidia sana katika kazi za usimamizi washughuli za uvuvi. Pamoja na kazi nyingine mashirika hayo yana kazi zifuatazo:

a) Kusaidia vikundi vya usimamizi wa raslimali za uvuvi katika maswala ya uhifadhi, usimamizi endelevu na matumizi bora ya raslimali ya uvuvi
b) Kukuza ushirikiano na maelewano baina ya wadau kwa njia za ugani
c) Uwekezaji katika kuongeza thamani kwenye mazao ya uvuvi kwa misingi ya kukuza uchumi na kupunguza uharibifu wa samaki na mazao ya uvuvi
d) Upatikanaji wa ajira na uwekezaji katika sekta ya uvuvi

SURA YA TATU:

USIMAMIZI SHIRIKISHI WA UVUVI KATIKA BAHARI YA HINDI

Usimamizi shirikishi maana yake ni kwamba kunakuwa na utaratibu ambapo Serikali na wadau wengine wa sekta ya uvuvi kama vile wavuvi, wafanyibashara wa samaki, wachakataji wadogo, mafundi wa kutengeneza mitumbwi/boti, mashirika yasiyo ya kiserikali, watafiti, vyuo vinavyofundisha taalauma za maliasili, wawekezaji na wengine wanagawana majukumu na malaka ya kusimamia kazi za kulinda, kuvuna na kuendeleza raslimali za uvuvi. Ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi wa shughuli za uvuvi maana yake ni kwamba kunakuwepo na utaratibu ambao majukumu ya usimamiaji wa raslimali za uvuvi unakuwa chini ya Idara ya Uvuvi na Halmashauri za wilaya (Serikali) na watumiaji wa raslimali za uvuvi. Kwa maneno mengine kunakuwepo na ushirikiano na mgawanyo wa mamlaka katika kufanya kazi za usimamizi wa raslimali za uvuvi kati ya Idara ya Uvuvi na watumiaji wa raslimali ya uvuvi.

Haja ya kuwa na Usimamizi Shirikishi

Uchumi wa kijamii na thamani ya kibaiolojia katika raslimali za ukanda wa pwani inatishiwa na shinikizo la ongezeko la idadi ya watu, ukuaji wa viwanda, pamoja na ujenzi holela katika pwani na mwambao mwa bahari, matumizi mabaya ya fukwe, uvuvi usioendelevu nakadhalika. Matatizo hayo yote yamesababisha kupungua kwa bioanuai na raslimali zingine na pia ongezeko la matumizi mabaya ya ardhi na kuongezeka kwa umasikini kwa

watu wanaoishi ukanda wa pwani. Kwa hiyo hatua madhubuti za kusimamia raslimali za uvuvi na mazingira ni lazima zichukuliwe kwa nia ya kubadilisha hali iliyopo sasa.

Madhumuni ya Usimamizi shirikishi

a) Kuwahusisha wadau katika kuendeleza na kutekeleza sera
b) Kulinda, kusimamia na kuendeleza matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi na kutoa mamlaka kwa watumiaji wa raslimali za uvuvi
c) Kujenga uwezo wa jamii katika usimamizi wa rasilimali za ukanda wa pwani.
d) Kuimarisha maisha ya jamii
e) Kuhusisha jinsia katika usimamizi

Historia ya maendeleo katika usimamizi wa uvuvi

Kabla ya ukoloni hadi 1920	**Mwanzoni samaki walivuliwa kwa matumizi ya nyumbani, zana za uvuvi zilitengenezwa kwa kutumia vifaa vya asili na usimamizi ulikuwa wa kimila ukitegemea imani za asili.**
Kipindi cha ukoloni hadi mwishoni mwa miaka ya 1970	**Hatua za usimamizi zililenga kulinda samaki aina ya "Trout" kwenye mito na zililenga kulinda uvuvi wa kustarehesha wazungu na wahindi (Watawala wa Kikoloni).**
Sheria ya Uvuvi ya mwaka 1970, Kanuni za Uvuvi za mwaka 1973 na 1989	**Sheria hii ilitoa mamlaka kwa Watumishi wa Serikali katika Idara ya Uvuvi kusimamia raslimali za uvuvi** **Sheria ilijihusisha na kulinda na kusimamia raslimali za uvuvi kwenye maji chumvi na baridi. Watendaji wa Serikali walikuwa ndiyo pekee wa kusimamia na kutekeleza majukumu yote.**

Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake (1997)	**<u>Tamko la Sera Na. 12 kuhusu Ushirikishwaji wa Jamii</u>** **Kuboresha ushirikishwaji wa jamii za wavuvi katika kupanga, kuendeleza, kusimamia na kutumia raslimali za uvuvi.** **<u>Mikakati:</u>** **a) Kuhusisha jamii za wavuvi katika kuandaa na kutekeleza sera kupitia vyombo vyao vinavyowahusu yaani Halmashauri za Wilaya, vyama, Kata, Vijiji, vikundi vya kijamii nakadhalika** **b) Kukabidhi majukumu ya usimamizi wa mialo/bandari za kupokelea samaki na vifaa vinavyotumiwa kwa jamii za wavuvi** **c) Kuwezesha utungaji wa sheria ndogo ndogo zinazohusiana na sekta ya uvuvi ili kuboresha uvuvi na matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi**
Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005 zinazohusu usimamizi shirikishi	**Baadhi ya Kanuni za Uvuvi zinazohusu vikundi vya usimamizi wa raslimali za uvuvi** **a) Kila jamii ya wavuvi kwa kushirikiana na Serikali ya Kijiji watalazimika kuanzisha Kikundi vya Usimamizi shirikishi wa raslimali za uvuvi kwa lengo la kulinda na kutunza raslimali za uvuvi** **b) Kila mvuvi/mdau atajiunga na Kikundi hicho isipokuwa wavuvi wakubwa wenye viwanda/biashara** **c) Mvuvi ambaye hatajiunga na kikundi cha usimamizi wa raslimali hatapewa leseni ya kuvua samaki** **d) Kila mjumbe wa kikundi atalazimika kujaza fomu na kuonyesha uzito wa samaki, thamani na bei yake kila siku na atawasilisha takwimu hizo kwa Afisa Uvuvi wa eneo lake**

Misingi (Principles) ya Usimamizi Shirikishi

a) Wakati wa kuanzisha usimamizi shirikishi inashauriwa kwamba ni vyema kufahamu tabia za vikundi na mabadiliko yake, pia chunguza utamaduni na uchumi wa jamii za wavuvi katika eneo linalohusika.

b) Kuwatambua watumiaji halisi wa raslimali za uvuvi na mipaka ya maeneo wanayovuna raslimali hizo.

c) Vikundi vya Usimamizi wa raslimali za uvuvi lazima viundwe na wadau wote wa kijiji wenye sifa kwa kuwa ndio wanaoimiliki na kunufaika nazo. Pia, ndio wa kwanza kuathirika mara raslimali za uvuvi zikitoweka.

d) Vikundi vya Usimamizi wa raslimali za uvuvi vihusishwe katika **kuandaa na kufanya marekebisho ya Sheria na Kanuni** za uvuvi kwa ajili ya matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi.

e) Kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Uvuvi.

f) Vikundi vya Usimamizi wa raslimali za uvuvi vinatakiwa kufuatilia kuona kuwa watumiaji hawavunji Sheria na Kanuni nyingine za nchi zilizopo.

g) Vikundi vya Usimamizi wa raslimali za uvuvi vinalazimika kuandaa sheria ndogo ndogo za usimamizi wa raslimali za uvuvi pamoja na adhabu kwa wanaovunja sheria.

h) Serikali kutambua kuwa Vikundi vya Usimamizi wa raslimali za uvuvi vina haki ya kusimamia raslimali za uvuvi.

i) Ushikishwaji wa jamii ya wavuvi katika usimamizi wa raslimali za uvuvi unaongeza ufanisi katika usimamizi na unapunguza migogoro katika ukanda wa pwani. Pia, unaongeza ubora wa ukusanyaji wa takwimu na taarifa za uvuvi

j) Serikali kuacha kuvuruga kazi za usimamizi wa raslimali za uvuvi zilizobuniwa na jamii katika maeneo yao.

k) Serikali inahimizwa kusaidia Vikundi vya Usimamizi wa

raslimali za uvuvi kwenye miradi ya kiuchumi.

l) Kuanzisha njia ya mawasiliano na upashanaji habari kati ya wadau.

Faida ya Usimamizi shirikishi

a) Ni rahisi kutatua migogoro inayojitokeza baina ya wadau katika uvunaji wa raslimali za uvuvi na usimamiaji wa mazingira.

b) Kunakuwepo na mgawanyo wa gharama za uendeshaji na kwa hiyo Serikali inapunguziwa gharama za usimamizi wa kazi za uvuvi.

c) Wavuvi wanashiriki kwenye kupanga ili kuboresha au kuongeza tija kwenye matumizi na hifadhi ya raslimali za uvuvi kwa ajili ya uvuvi endelevu.

d) Wavuvi na Serikali wanakuwa tayari kugawana na kupeana takwimu katika kuboresha usimamizi wa mazingira na raslimali za uvuvi na kupanga mipango ya maendeleo.

e) Elimu asilia ya wavuvi juu ya raslimali za uvuvi na mazingira inatumika kuboresha ufanisi kwenye usimamizi wa raslimali za uvuvi na mazingira.

f) Kuimarisha mshikamano na kuaminiana kati ya wavuvi na Serikali.

g) Kuboreshwa kwa usimamiaji wa Sheria ya Uvuvi na Kanuni zake. Kwa kuwa wavuvi wanaweza kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Uvuvi na Kanuni zake kwa vitendo bila kumtegemea Afisa Uvuvi.

h) Kuhakikisha kuwa samaki na viumbe walio kwenye hatari ya kutoweka wanarudia katika hali yao ya kawaida. Vilevile hifadhi ya mazigira inaboreshwa.

i) Kutoa mamlaka kwa jamii ya wavuvi ili kutoa maamuzi ya busara ya usimamizi na uvunaji wa raslimali za uvuvi pamoja na mazingira.

j) Kuwawezesha wadau waone na kuamini kuwa raslimali za uvuvi ni mali yao.
k) Kuongeza ufanisi katika kusimamia utekelezaji wa Sheria za nchi na Sheria ndogo ndogo walizotunga wao wenyewe.
l) Kunakuwepo na motisha kwa wavuvi katika kuchukua hatua za muda mrefu za usimamizi wa raslimali za uvuvi.
m) Kunakuwepo na uhakika wa kurudi kwa bioanuai iliyotoweka au iliyoko kwenye hatari ya kutoweka
n) Kuwapa nguvu na ufahamu jamii ya wavuvi kutambua kuwa raslimali ya uvuvi ni mali yao

Maana ya Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi

Ni taasisi ya kijamii inayoundwa na jamii ya wavuvi na wakazi wa mwambao ambayo majukumu yake makubwa ni kulinda, kutunza, kufuatilia na kudhibiti raslimali za uvuvi na kuwa na mipango endelevu ya mazingira na kuiendeleza katika eneo lao kwa kushirikiana na Serikali.

Sifa za mjumbe wa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi

a) Lazima awe raia wa Tanzania.
b) Lazima awe mvuvi, mfanyibiashara wa samaki, mchakataji wa samaki au mdau msuka nyavu, mlaji wa samaki, mtengenezaji boti/mitubwi au mdau mwingine.
c) Lazima awe mkazi wa bandari/forodha inayohusika.
d) Lazima awe mkereketwa wa kutunza mazingira na mwenye bidii ya kuhifadhi raslimali za uvuvi na mazingira kwa ujumla.
e) Mwanaume na mwanamke anapaswa awe na umri unaozidi miaka 18.
f) Lazima awe mwaminifu, msema kweli, mtunza siri, mpenda

ushirikiano na kufanya kazi za vikundi na mchapa kazi.

g) Viongozi wa jadi/ wazee wenye busara katika vijiji au forodha wenye sifa hizi wanahimizwa wajiunge ili kutumia uzoefu na ushawishi wao katika kupata matokeo mazuri katika kusimamia raslimali za uvuvi.
h) Mjumbe awe tayari kufanya kazi za kujitolea kwa kuwa hakuna mshahara/malipo ya kudumu kutoka Serikalini au taasisi nyingine yoyote
i) Viongozi wajue jinsi ya kuwasiliana (kusoma na kuandika) kwa Kiswahili.

Kuunda Baraza na Uchaguzi wa Kamati Tendaji ya Vikundi vya usimamizi shirikishi wa raslimali ya uvuvi (BMU-Executive Committee)

Baada ya mikutano ya kuhamasisha jamii kufanyika, inapendekezwa kuwa wadau wapewe angalau mwezi mmoja wa kutafakari na kujadiliana wenyewe umuhimu wa kushiriki kwenye usimamizi shirikishi unaohusisha jamii. Ni muhimu wadau/wananchi wafikie muafaka katika masuala muhimu kama yalivyotajwa hapo juu kabla ya kuanzisha kikundi cha usimamizi wa raslimali za uvuvi katika eneo lao.

a) Jamii ya wavuvi katika kijiji/ forodha watajiandikisha ili kuunda Baraza la Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi (BMU Assembly).
b) Baraza la Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi chini ya Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji watachagua kidemokrasia viongozi wa Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi. Ikiwa wanachama waliojiandikisha wamefikia 2/3 ya wakazi wenye umri zaidi ya miaka 18 katika kijiji kinachohusika. Viongozi waliochaguliwa wataunda Kamati Tendaji (BMU Executive Committee) ambao ni Mwenyekiti, Katibu, Mweka Hazina,

Mtunza Bohari, na Mzee mmoja maarufu mkereketwa na wajumbe wengine 10 na kwa hiyo Kamati Tendaji itakuwa na wajumbe 15. Katika wajumbe 15 asilimia thelathini (30%) ni lazima wawe ni wanawake wa kijiji kinacho husika.

Majukumu ya Wajumbe wa Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi (Beach Management Unit - BMU)

a) Kushiriki katika doria kulingana na ratiba ya doria iliyokubaliwa na wajumbe wote /wadau wote wa Kikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi. Eneo la kazi litategemea ukubwa wa kijiji, uwezo wa kufikia jamii na mipaka mingine inayotambulika na utawala wa kijiji.
b) Kukataza uuzaji wa samaki wachanga, matumizi ya zana haramu, ukataji wa miti ya mikoko bila kibali, na kuendesha biashara ya samaki na mazao mengine ya baharini bila ya kuwa na leseni.
c) Kushiriki katika kusimamia usafi wa maji na mazingira kwenye forodha/bahari.
d) Kushiriki katika kuandikisha boti/mitumbwi yote katika forodha/mwalo.
e) Kushiriki na kuhakikisha kuwa wavuvi wote wanakata leseni zao za uvuvi na za vyombo vyao vya uvuvi kila mwaka.
f) Kuhakikisha kuwa zana zote za uvuvi zilizopigwa marufuku zinasalimishwa kwenye mamlaka zinazohusika ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, viongozi wa Kamati Tendaji ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi, Afisa Mtendaji wa Kijiji, Afisa Mtendaji wa Kata, Afisa Uvuvi na Afisa Maliasili wa Wilaya na Mkoa.
g) Kushiriki katika mchakato wa kuandaa mpango wa kusimamia maeneo ya uvuvi ya pamoja ambayo yanavuliwa na wanavijiji wa vijiji tofauti. Maeneo hayo ni lazima yanapangiwe utaratibu muafaka wa usimamizi wa

pamoja kwa manufaa ya wananchi wanaohusika.

h) Kutekeleza mpango/mipango ya kazi itakayo pangwa na jamii yenyewe kuhusu masuala ya uvuvi na mazingira **(Kiambatanisho Namba 1- 3)**.

Majukumu ya Baraza la Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi (Mkutano Mkuu wa wajumbe wote)

a) Baraza lina mamlaka ya juu na linatoa maamuzi ya mwisho.
b) Baraza lina mamlaka ya kuchagua na kumuondoa kiongozi au wajumbe wa kikundi husika.
c) Baraza litaidhinisha mipango ya maendeleo ya usimamizi wa shughuli za uvuvi baina ya vijiji kwa ajili ya usimamizi wa pamoja katika maeneo ya mavuvi yanayotumiwa na zaidi ya kijiji kimoja (maeneo ya mavuvi ya pamoja).
d) Kuidhinisha miradi ya kiuchumi pamoja na maeneo ya vyanzo vya mapato na matumizi ya mapato **(Kiambatanisho Namba 6-7)**
e) Kuidhinisha mipango ya usimamizi na kazi (maendeleo), bajeti, taarifa za ukaguzi wa mahesabu.
f) Kuidhinisha sheria ndogo ndogo zilizoandaliwa na Kamati Tendaji kwa ajili ya kuziwasilisha katika Serikali ya Kijiji kwa hatua za utekelezaji

Majukumu ya Kamati Tendaji (BMU Executive Committee)

a) Kamati Tendaji imepewa madaraka ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za uvuvi kwa niaba ya Baraza la Kikundi cha Usimamizi wa raslimali za pwani za eneo/kijiji husika
b) Kuweka rejesta/kumbukubu za wadau na matukio ya kila siku **(Kiambatanisho Namba 1 - 3)** ikiwa ni pamoja na wamiliki wa mitumbwi, wavuvi, na zana zao na wajumbe wa BMUs katika forodha inayohusika kwa kushirikiana na

Kamati nyingine za Kijiji, Serikali za vijiji, Halmashauri za Wilaya na Serikali Kuu.

c) Kufanya maamuzi ya aina za alama za kuweka kwenye zana (vyombo, mashine na mitego ya uvuvi) ili zitumiwe katika kusaidia kudhibiti matukio yasiyofaa na kuleta ufanisi katika kazi (Mfano katika kufuatilia masuala ya wizi wa zana za uvuvi).

d) Kushiriki katika kufanya maamuzi ya wavuvi wanaostahili kupewa leseni za vyombo na zana za uvuvi kwa kushirikiana na Maafisa wa Serikali ili kuhakikisha kuwa wanaopewa leseni wameshajiandikisha kuwa wajumbe wa Vikundi cha Usimamizi wa raslimali za uvuvi katika pwani na bahari.

e) Kuteua maeneo ya mazalia ya samaki kwa kutumia elimu asilia na sayansi na kuhakikisha kuwa maeneo ya mazalio hayavuliwi.

f) Kuteua maeneo kwa ajili ya mavuvi na usimamizi wa pamoja (Collaborative Fisheries Management Areas - CFMAs) wa raslimali za bahari na pwani baina ya vijiji vya karibu na kuyasimamia kulingana na makubaliano ya wadau.

g) Kuandaa ratiba ya doria na kusimamia kazi zote za BMU kwa kushirikiana na Serikali.

h) Kuratibu kazi za kukusanya takwimu za mavuvi ya kila siku (Catch Assessment Surveys) na sensa ya mavuvi ("frame surveys"), hali ya uvuvi katika maeneo yao, na kuasaidia katika tafiti mbalimbali za kibaologia na kijamii kwa kutumia utaratibu uliokubalika.

i) Kukagua na kuweka kumbukumbu za wavuvi wageni na boti zao na kutoa kibali cha kuingia kwenye bandari/forodha.

j) Kudhibiti wavuvi wahamiaji na kuhakikisha kuwa wanafuata sheria za nchi na sheria ndogo ndogo za BMU na kijiji husika.

k) Kusimamia usafi wa mazingira na ubora wa mazao ya

samaki kwenye forodha/bahari.

l) Kuimarisha mtandao wa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi ili kufanikisha upeanaji wa habari na taarifa ulio thabiti (mfano biashara, uthibiti wa majina ya wavuvi waharibifu, uwekaji wa bei za samaki na mazao yake unaozingatia haki), usimamizi ya raslimali za uvuvi na usalama wa watu na mali zao.

m) Kamati Tendaji ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi inawajibika kuaandaa mpango kazi unaotokana na mpango wa usimamizi wa kikundi husika kwa ajili ya maendeleo katika maeneo yao na kuhakikisha kuwa unatekelezwa. Pamoja na kubuni njia mbadala za mapato na matumizi ya mapato **(Kiambatanisho Namba 6 -7)**

n) Kuandaa mipango ya mwaka, bajeti na kuwasilisha kwenye Baraza la Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi kwa ajili ya kupata idhini ya utekelezaji

o) Kuandaa michanganuo ya miradi kwa ajili ya kuboresha kipato na matumaini ya kudumu kwa vikundi hivyo na kuwasilisha kwenye Baraza la Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi ili kupata idhini ya utekelezaji.

p) Kuwakilisha michanganuo hiyo kwa wahisani, Miradi ya mazingira, Halmashauri za Wilaya na Idara ya Uvuvi

q) Kusimamia utekelezaji wa mipango ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi

r) Kamati Tendaji inawajibika kufuatilia kazi zote za kila siku za wadau wote katika forodha/bandari

Mikutano ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi

a) Baraza la Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi litakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu

b) Baraza la Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali

za uvuvi litakuwa na Mkutano Mkuu wa mwaka kutathimini masuala mbalimbali na kutoa maamuzi mazito yanayohusiana na kipindi cha mwaka mzima

c) Kamati Tendaji itakutana mara moja kwa mwezi
d) Kamati Tendaji itakuwa na mikutano ya dharura mara itakapo bidi kufanya hivyo

Majukumu ya Mwenyekiti

a) Kiongozi Mkuu wa Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
b) Kusimamia kazi zote na mikutano yote ya Baraza na mikutano ya Kamati Tendaji
c) Msemaji wa Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
d) Anaidhinisha masuala yote ya fedha za Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi

Majukumu ya Katibu wa Kamati Tendaji

a) Kuandaa mikutano baada ya kujadiliana/kuwasiliana na Mwenyekiti
b) Katibu wa mikutano ya Baraza na Kamati Tendaji ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
c) Mtunza kumbukumbu za mikutano na barua/mawasiliano yote ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
d) Kuandaa taarifa za kazi za mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mmoja na kuziwasilisha kwenye Baraza la Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi **(Kiambatanisho Namba 1-3)**
e) Kutunza kumbukumbu sahihi za wajumbe wote wa Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi, wavuvi, na wadau husika wa uvuvi, vifaa, takwimu nakadhalika

Majukumu ya Mweka Hazina

a) Kuandaa na kufanya malipo yaliyoidhinishwa na Kamati Tendaji ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
b) Kutunza kumbukumbu za masuala ya fedha na vitabu vya hesabu za Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
c) Kupokea fedha taslimu na kuweke fedha benki kwenye akaunti ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
d) Kutunza vifaa vyote vinavyohusiana na ofisi ya mweka Hazina
e) Kuandaa taarifa za fedha za mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mmoja kwa ajili ya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi (matumizi na mapato)
f) Kuwasilisha taarifa/matumizi, mahitaji ya fedha kwenye Kamati Tendaji na Baraza la Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi kwa kupitia na kupata idhini

Majukumu ya Mtunza Bohari

a) Msimamizi wa kazi zote za bohari zinazomilikiwa na jamii
b) Kupokea maombi ya mikopo, kutoa mahitaji ya ofisi na vifaa
c) Kutunza kumbukumbu, risiti, mikopo na vifaa viliyotolewa kwenye bohari
d) Kuwasilisha taarifa za bohari kwenye Kamati Tendaji na Baraza la Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
e) Kutunza vifaa na vitu vingine vya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi

Kamati ndogo za Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi

Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi vitawajibika kuanzisha Kamati ndogo ndogo zifuatazo:

a) Kamati ndogo ya udhibiti na doria
b) Kamati ndogo ya fedha na uzalishaji mali
c) Kamati ndogo ya kukusanya taarifa (takwimu) na habari na kuzisambaza kwa wadau mbalimbali

Kamati hizo ndogo zitaundwa na wajumbe wasiopungua watano (5). Wajumbe hawa watachaguliwa na Baraza la Kikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi. Kila Kamati ndogo itakuwa na asilimia thelathini (30%) ya wajumbe wake ambao ni wanawake. Jedwali lifuatalo linaonyesha kamati hizo katika ngazi ya kijiji

JEDWALI LINAONYESHA MUUNDO WA KIKUNDI CHA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA RASLIMALI ZA UVUVI KATIKA NGAZI YA KIJIJI



Wajumbe kukosa sifa

Mdau yeyote atakosa sifa za kuwepo kwenye Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi ikiwa atafanya yafuatayo:

a) Akijihusisha na uvuvi haramu au vitendo vingine vya kuvunja Sheria na Kanuni za Uvuvi
b) Akionyesha tabia inayokiuka madhumuni ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
c) Akipatikana na hatia ya kushiriki kwenye uvuvi haramu na kuvunja sheria ndogo ndogo za Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
d) Akionekana sio mwaminifu na akipatikana na hatia ya kuvunja Sheria na Kanuni za Uvuvi na Sheria nyingine za nchi za hifadhi ya raslimali za uvuvi na mazingira
e) Akikosa sifa za kufanya kazi za pamoja na jamii na kuwa sio mpenda maendeleo
f) Akiwa hakubaliki na jamii kutokana na sababu ambayo jamii kwa pamoja itakuwa imeainisha kulingana na sheria ndogo ndogo zilizopangwa, mila na desturi za mahali pale
g) Akichanganya masuala ya usimamizi shirikishi wa raslimali za pwani na bahari na siasa kwa lengo la kupotosha dira ya dhana hiyo kwa jamii

Muda wa Viongozi kukaa madarakani

Viongozi na wajumbe waliochaguliwa wa Kamati Tendaji na Kamati ndogondogo watakaa madarakani kwa muda wa miaka mitatu (3) na wanaweza kuchaguliwa kwa mara ya pili na baada ya hapo hawatagombea tena kwa ajili ya kutoa nafasi ya uongozi kwa wadau wengine wa Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi.

Afisa Uvuvi wa eneo linalohusika anawajibika kutoa ufafanuzi

katika masuala mbalimbali katika jamii ya wavuvi ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri na kufuatilia kazi za Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi na kutoa kila aina ya msaada pale inapowezekana ili kuimarisha vikundi husika. Pia, anawajibika kuandaa taarifa za utekelezaji za robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mmoja **(Kiambatanisho Namba 4 -5)** na kuziwasilisha kwa Mkurugenzi wa Uvuvi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya.

Muundo wa Utawala

Sheria iliyoanzisha Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 imetoa mamlaka kwa Serikali za Vijiji kuanzisha Kamati mbalimbali katika Serikali ya Kijiji ili kuboresha, kuongeza ufanisi na tija katika kazi mbalimbali zinazofanyika kwenye kijiji. Kutokana na hali hiyo Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi ni Kamati ndogo ndani ya Kamati ya Serikali ya Kijiji iliyochaguliwa na Serikali ya Kijiji kinachohusika.

Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi vitakuwa katika ngazi ya kijiji chini ya Kamati iliyochaguliwa na Serikali ya Kijiji

Kwa upande mwingine Idara ya Uvuvi na Halmashauri za Wilaya zinafanya kazi kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji kwa kupitia Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi. Pia, Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 katika kifungu cha V imetoa mamlaka ya kisheria kwa Serikali za vijiji kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi.

Utaratibu wa kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi

a) Kuteua waraghabishi (Change Agents) kutoka ngazi ya wilaya kwa kufuata vigezo maalum (Mfano awe mwajiriwa wa kudumu katika Halmashauri, awe mtaalam katika fani ya uvuvi, misitu na nyuki, wanyamapori, kilimo, maendeleo ya jamii, ualimu) au awe mtaalam mwajiriwa wa mradi uliopo wilayani.
b) Kutoa mafuzo juu ya dhana ya usimamizi shirikishi ya uvuvi kwa watendaji wa Halmashauri ya wilaya
c) Kutoa mafunzo kwa asasi mbalimbali zisizo za kiserikali na viongozi wa dini kwa ushirikiano na watendaji wa wilaya
d) Kutoa mafunzo ya uanzishwaji wa vikundi hivyo katika ngazi za vijiji na kuchagua waragabishi katika ngazi hiyo.
e) Katika kutekeleza jukumu la (d) hapo juu, waraghabishi wa ngazi za vijiji watateuliwa kwa kufuata sifa kadhaa ikiwa ni pamoja na:- Wawe wanajua kusoma na kuandika; Wakereketwa wa kutunza raslimali za uvuvi/bahari na pwani; Wakazi wa kijiji husika; Wawe na umri usiopungua miaka 18; Wawe tayari kufanya kazi za kujitolea.
f) Waragabishi/Waelimishaji wa ngazi ya kijiji wataunda timu maalum ya uelimishaji katika ngazi ya vijiji vyao hasa baada ya kupata elimu kutoka kwa wataalam wa ngazi ya taifa na wilaya na kuelewa mambo yaliyojiri katika sehemu (d) hapo juu
g) Afisa Mtendaji wa Kata (Ward Executive Officer-WEO) na Afisa Mtendaji wa Kijiji (Village Exuctive Officer –VEO) wataungana na waragabishi wa ngazi ya vijiji katika kupata mafunzo ya usimamzi shirikishi. Pia mikakati ya kuendesha zoezi la uanzishaji wa BMU itajadiliwa ili kupata uzoefu wa kutataua masuala yatakayojiri wakati wa mikutano ya kijiji

katika sehemu (d) hapo juu.

h) Afisa Mtendaji wa Kata na Afisa Mtendaji wa Kijiji wataitisha mikutano ya viijiji na kupanga tarehe maalum ya kuendesha uchaguzi wa viongozi wa BMU katika maeneo yao. Katika ngazi hii Idara ya Uvuvi, Taasisi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali, Wataalamu wa Miradi, Mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile WWF nakadhalika hawatakuwa mstari wa mbele bali wanaweza kualikwa kusikiliza mambo yanayoendelea kwa vijiji vitakavyopenda kutoa mialiko hiyo.

i) Mchakato wa kuendeleza elimu ya usimamizi shirikishi katika ngazi za vijiji utasimamiwa na Afisa Mtendaji wa Kata na Afisa Mtendaji wa Kijiji kwa wakishirikiana na Halmashauri za Wilaya na Vijiji kwa kupitia mikutano ya hadhara.

j) Baada ya hapo, watu kwa matakwa yao (wadau wote kijijini) watajiandikisha kwa lengo la kuwa wanachama/wadau kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji husika chini ya usimamizi wa Afisa Mtendaji wa Kata .

k) Maombi ya kuomba uongozi wa BMU yatafanyika kabla ya siku ya uchaguzi na kuwasilishwa kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji na baada ya hapo uchaguzi utafanyika wa viongozi wa Kamati Tendaji na wa Kamati Ndogo kwa uhuru na uwazi.

l) Uchaguzi na uanzishwaji wa BMU utafanyika baada ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya kufanyika mkutano wa hadhara katika kila kijiji/eneo husika na baada ya watu kuelewa dhana ya usimamizi shikishi na mchakato mzima wa kuanzisha BMU.

m) Baada ya uchaguzi wa viongozi wa BMU, Halmashauri za Vijiji, Kamati Tendaji za BMU na Kamati Ndogo za BMU, makundi maalum katika jamii (wanawake, vijana, wazee) vitaimarishwa kwa kupewa mafunzo na nyenzo mbalimbali kulingana na mahitaji na uwezo wa uwezeshaji

wa Halmashauri za Wilaya, Serikali Kuu na wafadhili. Hii ni kazi itakayo fanywa kwa vipindi tofauti kulingana na haja hiyo.

n) Hati ya kuandikishwa ya BMU itapatikana (Certificate of Registration) baada ya uongozi wa BMU kutoa maombi kwa Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi kwa kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hamashauri ya Wilaya inayohusika

o) Kuandaa mpango wa usimamizi na mpango wa kazi wa kusimamia raslimali za pwani na bahari katika ngazi ya kijiji

p) Kuanzisha mchakato wa kuangalia maeneo ya mavuvi na usimamizi wa pamoja (Collaborative Fisheries Management Areas - CFMAs). Zoezi hilo litafanyika mara baada kuanzishwa kwa BMU katika kila kijiji na kuaandaa mpango wa usimamizi kwa kila kijiji (Management Plan)

q) Ufuatiliaji wa mwenendo wa kazi za BMU utafanywa kwa pamoja na ikibidi kwa kutumia wataalamu wengine ili kuboresha kazi na muundo mzima wa BMUs. Zoezi hili la ufuatiliaji litafanywa zaidi na wataalam katika ngazi ya wilaya na kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Uvuvi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya inayohusika na wafadhili.

MCHAKATO WA UANZISHWAJI WA VIKUNDI VYA USIMAIZI SHIRIKISHI WA RASLIMALI ZA UVUVI.



Majukumu ya Msimamizi wa Uchaguzi wa Kamati Tendaji na Kamati ndogo ya Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi (BMU)

Majukumu ya Msimamizi wa Uchaguzi

Hapa Tanzania Msimamizi wa Uchaguzi ni Afisa wa Serikali ambaye yuko huru na hafungamani na upande wowote na anatumia madaraka aliyopewa kufanya kazi zake kwa uhuru bila kufungamana na chama chochote cha siasa au kundi la kijamii lililopo mahali husika. Katika hali hiyo Maafisa Watendaji wa Kata na Maafisa Watendaji wa Vijiji watakuwa wasimamizi wa uchaguzi katika Kata na Vijiji vyao ili kuhakikisha kuwa Vikundi vya Usimamizi wa raslimali za uvuvi vianaazishwa chini ya mfumo wa Serikali za Vijiji. Katika mchakato mzima wa uanzishaji wa BMU, Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji watakuwa na dhamana hiyo. Kwa hivyo majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kata ni kuratibu kazi za Maafisa Watendaji wa viijiji katika Kata yake. Kwa hivyo Maafisa Watendaji wa Vijiji watakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kuratibu mchakato wa kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi katika vijiji
b) Kuratibu uhamasishaji na uelimishaji wa jamii ya watu wa pwani katika kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
c) Kuwaandikisha wadau wote muhimu katika kijiji kabla ya kuchagua viongozi wa Kamati Tendaji ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi
d) Kutunza rejista ya wajumbe wote wa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi katika ngazi ya Kijiji na kutoa nakala katika ngazi ya Kata na kuhakikisha kuwa rejista hiyo inapewa Kamati Tendaji ya Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi katika kijiji

husika mara tu baada ya uchaguzi kufanyika

e) Kuratibu kampeni za uchaguzi wa viongozi wa BMU na kuwa Mkuu wa protokali/utaratibu uliowekwa unafuatwa katika kijiji (Afisa Mtendaji wa Kijiji)

f) Kusimamia uchaguzi wa viongozi wa BMU

Majukumu Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji

Baada ya kuundwa kwa Baraza la BMU na kuchaguliwa kwa Kamati Tendaji na Kamati Ndogo za BMU Maafia Watendaji wa Kata na Vijiji watakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kusimamia mahusiano mazuri baina ya Kamati Tendaji ya Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi, Serikali ya Kijiji na Kamati ya Maendeleo ya Kata

b) Kuratibu uandaaji wa ripoti za Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi katika kijiji (Afisa Mtendaji wa Kijiji) na kata (Afisa Mtendaji wa Kata) na kuwasilisha ngazi za juu yake kama vile Tarafa, Wilaya, Mkoa, Idara ya Uvuvi na waratibu wa miradi husika itakayo fanya kazi pamoja na vikundi hivyo kama vile WWF, MACEMP nakadhalika

c) Afisa Mtendaji wa Kata ataitisha na kuandaa mikutano yote kwa ajili ya kutengua ujumbe wa mdau yeyote wa Kamati Tendaji ya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi baada ya kupokea mapendekezo theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wote wa Kikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi

d) Afisa Mtendaji wa Kata ataandika barua ya onyo na kutengua ujumbe katika kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi baada ya mjumbe kukosa sifa au kosa jingine lisilokubalika na BMU inayohusika.

SOMO LA NNE:

UONGOZI NA UTAWALA BORA

Uongozi na Utawala Bora

Maana ya Kiongozi: Kiongozi ni mtu yule ambaye ana uwezo wa kuonyesha njia wenzake na kuwaongoza kwa tahadhari ya kutoleta madhara au migongano katika eneo/sehemu anayowaongoza.

Aina za Uongozi

a) **Demokrasia:** Ni uongozi unaohakikisha uhusikaji wa watu na maamuzi ya waliowengi katika kutekeleza mambo na masuala mbali mbali.

b) **Dikteta (utawala wa kiimla):** Ni utawala ambao mtu huchukua mawazo yake pekee katika kuamua masuala mbali mbali na kutegemea kukubalika kwa mawazo hayo kwa kupata upinzani mdogo au bila kupingwa kabisa.

c) **"Laissez-faire" - Kiongozi asiyejali (Havinimbi):** Ni neno la kifaransa lenye kumaanisha kiongozi ambaye yupo lakini ni kama hayupo, asiye makini, anayekubali kila jambo na kila wazo bila yeye kuwa na uwezo wa kuchangia chochote. Anaweza kuruhusu watu kufanya majukumu yao kwa usimamizi mdogo toka kwake.

Kiongozi bora

a) Husikiliza mawazo ya watu

b) Anachambua matatizo na anatafuta njia za jinsi ya kutatua matatizo
c) Anafanya maamuzi yanayo tukuza maslahi ya wengi na sio kundi la watu wachache
d) Anahusisha wenzake katika maamuzi
e) Anatumia nyenzo mbalimbali katika kufanya maamuzi (tafiti, vikao n.k)
f) Anaacha nafasi iwapo agenda haikubaliki
g) Anajihusisha katika masuala ya vikundi
h) Muwazi, muwajibikaji na mbunifu
i) Mwenye uwezo wa kushawishi, mwenye mapenzi na watu na mbunifu
j) Mwenye upeo wa kuona mbali na mikakati mizuri ya utendaji kulingana na upeo huo
k) Mwenye uwezo wa kujitoa muhanga
l) Mtu mwenye mawasiliano mazuri na watu na mwenye kujiamini
m) Anajizatiti, mwenye nguvu na uwezo wa kuwezeshwa kupanga na kutekeleza yanayotarajiwa

Kiongozi makini:
a) Analeta hamasa katika utendaji wa kazi
b) Baada ya kupima na kuchambua hutumia maarifa kuchochea utendaji mzuri wa kazi
c) Hufanya mawasiliano ya kutosha kabla ya kufanya maamuzi
d) Hupenda kuhamasisha mambo ya vikundi kwa ajili ya kuinua maisha ya watu wa hali ya chini
e) Husaidia na kuwezesha vikundi na kuwafanya wasiwe na hofu wakati wa kutoa maoni
f) Hutoa madaraka kwa walio chini kwa kutokujichosha na kujenga uwezo kwa wale anaofanya nao kazi

g) Ni mtu anayepanga mipango kwa kuzingatia sera, hupanga mbinu za utekelezaji na kupanga mipango ambayo inaleta manufaa ya baadae
h) Mtu anayependa kufanya kazi kwa kujenga timu mzuri katika sehemu ya kazi

Maana ya Utawala bora: Ni aina ya utawala ambao unafuata Demokrasia, haki za binadamu, maadili, uwazi na mikakati thabiti ya mipango inayotekelezeka. Unafuata na kuheshimu mawazo ya watu katika kutoa maamuzi mbalimbali. Utawala bora hutoa madaraka na mamlaka katika ngazi mbalimbali za utendaji na unaheshimu na kuafiki ushiriki wa watu katika kupanga, kutekeleza na kutathmini matokeo. Kifupi ni hali ambayo maamuzi yanafanywa na watu kwa maslahi ya watu na sio mtu au kikundi cha watu.

Kanuni na Misingi ya Utawala Bora:

a) **Demokrasia:** Ni utawala ambao viongozi wanachaguliwa na maamuzi yanatolewa kwa haki na usawa. Katika aina ya utawala huu, watu wanakuwa na matakwa ya kumchagua kiongozi wanayemtaka na kutoa mawazo yao bila woga. Kwa kuwa utawala huu una mizizi katika serikali, lazima taratibu na maadili kadhaa yafuatwe. Kati yake ni haya yafuatayo:
   i) Nidhamu na uadilifu
   ii) Utekelezaji kufuata maamuzi ya wengi
   iii) Kutumia vigezo na taarifa mbalimbali katika kutoa maamuzi
   iv) Kuwa tayari kutofautiana lakini sio kugombana
   v) Kuwa tayari kukosolewa bila kuficha ukweli

b) **Utawala wa sheria:** Utawala bora hufuata misingi ya sheria na unafuata Katiba ya Nchi, Sheria na Kanuni na taratibu

nyingine zilizokubalika. Kiongozi bora hapaswi kutawala kupita pale sheria inavyosema (beyond the rule of law). Maamuzi hayafanywi kinyume na Sheria ililyopo.

c) **Haki na usawa:** Katika utawala bora haki ni msingi katika maamuzi ili kuondoa upendeleo na kutokufuata haki katika jamii. Katika utawala wa misingi hii, kuaminiana na imani baina ya watu ni suala la msingi sana. Ni muhimu kwa kiongozi kutambua kuwa haki za watoto, wazee, wanawake na wanaume zinafuatwa.

d) **Ushiriki wa watu:** Maendeleo endelevu huletwa na watu wenyewe na sio viongozi au wafadhili. Kinachotakiwa kufanywa na viongozi ni kuhakikisha kuwa kuna ushirikishwaji wa kutosha wa jamii ili mradi unalenga kuboresha maisha yao. Ili kufanikisha adhima hii ni lazima kiongozi afanye vikao katika eneo lake la kazi, awe anakubali mazungumzo ya ana kwa ana na watu katika ngazi mbali mbali. Ili kuhakikisha utawala bora unafuatwa, yafuatayo yanapendekezwa kizingatiwa na uongozi katika ngazi ya kijiji:
   i) Mikutano na wakazi wa mtaa - mara moja katika miezi miwili
   ii) Mikutano na wakazi katika kitongoji – mara moja kwa mwezi
   iii) Mikutano na wakazi katika kijiji – mara moja katika muda wa miezi mitatu

e) **Ukweli, uwazi na uadilifu:** Kiongozi yeyote anatakiwa kuongoza watu na sio kuwaburuza watu. Kiongozi anatakiwa kuwa karibu na watu, kupata mawazo na mbinu za utendaji kazi na kutoa marejesho kwa kila

jambo linalotokea na kuamuliwa katika ngazi inayopaswa kupata taarifa hiyo. Katika kutekeleza masuala mbalimbali kiongozi lazima awe muwazi na mkweli kwa watu kuelewa kinachoendelea.

f) **Uchapa kazi:** Utawala bora hufuata misingi dhabiti ya watu kuchapa kazi na sio kutegemea misaada au kupata bure. Hii ni katika kuwa na msimamo katika maamuzi na umiliki wa matunda yatokanayo na kazi na juhudi katika utendaji mzima wa kazi. Katika hili hiyo, utawala bora hujenga uwezo, hujenga umiliki wa matunda ya kazi na hujenga imani na matumaini ya kuwa na maisha bora.

Wajibu wa wananchi ili kuwa na utawala bora

a) Kushiriki kwa dhati katika shughuli zote za kiuchumi na kijamii
b) Kugombea uongozi na kupiga kura kwa wengine pia
c) Kujifunza na kuelewa Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni, mila na taratibu ili kutumia haki kikamilifu
d) Kupenda amani, utulivu na maamuzi ya pamoja

Jukumu la Kiongozi chini ya mfumo wa utawala bora

a) Lazima kiongozi aelewe kuwa mfumo wa vyama vingi unaleta ushindani ili kuleta mafanikio zaidi na sio unavuruga taratibu anazotaka yeye na viongozi wenzake
b) Lazima aelewe aina ya vyama vyote vilivyopo katika eneo lake analoongoza
c) Kuhakikisha kuwa kazi zote zinazotekelezwa na Serikali zinafanywa kwa kufuata misingi ya Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa na kukubalika.

SOMO LA TANO:

JINSI YA KUTATUA, KUZUIA NA KUHIMILI MIGOGORO

Maana ya migogoro

Migogoro ni hali ambayo inajitokeza wakati mtu/kikundi au jamii inapokuwa na maoni tofauti juu ya jambo fulani na kila pande kuwa na hali ya kung'ang'ania fikra au matakwa yake. Kawaida migogoro inaambatana na mambo yafuatayo:

a) Hali inayosababisha pande moja kutotoa nafasi kwa upande mwingine na kutoa maoni na mawazo yake binafsi
b) Hali ambayo husababisha kuwa na pengo kubwa katika kupata mafao/manufaa au faida ya jambo fulani
c) Hali ambayo mtu anaweza kuwa anafanya kazi fulani ambayo haitambuliwi au haikubaliki na jamii anayoifanyia kazi
d) Hali ambayo inasababisha taarifa kutofika kwa jamii inayohusika kama inavyopaswa
e) Hali ambayo inakuwa ya ubabe katika maamuzi ya mambo mbalimbali
f) Hali ambayo kikundi au mtu binafsi hung'ang'ania jambo kwa lengo la kufurahisha kikundi au watu wachache kwa maslahi ya watu wachache au mtu binafsi

Sababu za kuwepo migogoro hasa katika sekta ya maliasili ambapo jamii humiliki raslimali kwa pamoja:

- Watu wachache wenye nguvu za kisiasa, kiuchumi na kijamii kuburuza wachache wasionacho, wanyonge na masikini
- Elimu duni na kutokuwa na uelewa katika mambo ya

kutunza, kumiliki na kutumia maliasili

- Kutokuwa na uwazi katika maamuzi mbalimbali
- Kuwepo kwa matabaka mbalimbali katika jamii kiuchumi, kisiasa na kijamii
- Kupungua kwa maliasili kama raslimali inayotegemewa na wanyonge
- Kutokuwa na raslimali mbadala na hivyo kutegemea raslimali ya aina moja
- Kuwa na hali isiyokuwa na vikwazo katika kuvuna raslimali hivyo kufaidisha wachache
- Kutokuwa na mipaka ya matumizi katika kuvuna na kulinda maliasili
- Kuwepo kwa vipato tofauti katika mavuno ya maliasili
- Kuwepo kwa wahamiaji wasiofuata sheria zilizowekwa katika maeneo tofauti
- Kuwepo kwa wahamiaji wasiofuata mila na desturi zilizowekwa na jamii
- Umasikini uliokithiri katika jamii
- Kutofuata haki za kijinsia na kuwa na hali ya ukandamizaji katika jamii
- Ubinafsi, upendeleo na kutojali matakwa ya walio wengi
- Kutokuwa na haki na muundo unaoeleweka katika umiliki wa maliasili
- Kutokuwepo kwa nguvu za kisheria katika jamii
- Kuwepo kwa sheria za ukandamizaji wa baadhi ya vikundi katika jamii
- Kutokuwepo kwa haki katika kugawana mapato
- Kutokuwepo kwa uainishaji wa majukumu mbali mbali na wahusika wa utekelezaji wa majukumu hayo
- Kuchanganya itikadi za dini na siasa katika suala la utunzaji, maendeleo, usimamizi na matumizi ya maliasili.

Jinsi ya kutatua migogoro na migongano katika kutumia raslimali za jamii

- Hakikisha kuwa kunakuwepo kwa vikao, mikutano na majadiliano ya mara kwa mara
- Hakikisha kuwa jamii husika zinapata fursa ya kusikilizwa matakwa yao
- Kutambua kuwa jamii husika zina mambo yanayowiana na yasiyowiana ili kuleta ushirikiano na maelewano.
- Hakikisha kuwa pande zote zimeeleza matakwa na malengo yao na pia uwezekano wa kuwa na njia mbadala ya kufikia hayo malengo na matakwa yao na sio wanavyofikiri wao tu.
- Hakikisha kuwa tatizo kubwa linatatuliwa kwa awamu ili kufanya majadiliano na makubaliano kuwa mapesi
- Kukutana na pande zinazohusika kwa wakati tofauti ili kuelewa undani wa mambo kwa urahisi na jinsi ya kuyatatua.
- Jaribu kuomba msaada toka nje kwa wengine kusaidia kutatua matatizo iwapo inakuwa ngumu kwa wenyewe kufanya hivyo
- Hakikisha kuwa kuna utunzanji wa taarifa na upelekaji wa taarifa hizo kwa jamii unafanyika kwa wakati muafaka.

Jinsi ya kutatua, kuhimili na kuzuia migogoro na migongano

- Kutumia mazungumzo/ vikao: Ni hali ambayo pande husika hukutana ana kwa ana na kuamua kufanya majadiliano
- Kutumia usuluhisho: Ni hali ambayo mazungumzo hufanywa na mtu wa tatu anayetoka upande usiofungamana na upande wowote katika harakati za kupunguza migogoro
- Kutumia upatanisho: Ni hali ambayo mazungumzo

hufanywa kwa hali ya kuleta upatanishi kama agenda kuu na sio kutaka kumfurahisha kila mmoja na ajenda yake. Jambo kuu linalo angaliwa hapa ni kupatanisha na hatimaye kuondoka katika hali ambayo pande zote zimeridhia.

- Kuepuka: Jaribu kuepuka hasa mtu au jamii inapokuwa ina hasira panahitajika muda ili hasira ipungue na suala litatuliwe.
- Kukubaliana: Iwapo suala sio muhimu sana kwa jamii au kikundi husika toa nafasi kwa suala jingine kuzungumziwa ili kumaliza la kwanza.
- Kulazimisha: Wakati panahitajika maamuzi ya haraka kwa maswala yenye umuhimu inabidi utumie mbinu ya kulazimisha pale inapobidi.
- Muafaka: Panahitajika muda katika masuala magumu hasa pande zote mbili zinapokuwa na nguvu. Mbinu mbali mbali zinahitajika katika hali hii na hasa zile zitakazozuia migogoro kuwa mikubwa.
- Ushirikiano: Ni wakati ambapo suala husika ni la muhimu sana kufikia muafaka kwa maslahi ya wengi na isipofanyika hivyo inaweza kuleta madhara katika jamii.
- Hamasisha/shawishi: Utaratibu wa kuhakikisha kwamba unashawishi wahusika vyakutosha ili wakubaliane na jambo ili kuzuia migogoro. Uhamasishaji huo uwe unalenga maslahi ya wengi na sio wachache.

SOMO LA SITA:
VIASHIRIA KWA AJILI YA USIMAMIZI SHIRIKISHI KWENYE RASLIMALI ZA PWANI NA BAHARI

VIASHIRIA VYA MAFANIKIO YA UTOAJI ELIMU YA KUANZISHA BMUs (*OUTPUT INDICATORS)*

Kiashiria	Taarifa z a awali	Mwaka 1	Mwaka 2	Mwaka	Mwaka 4	Mwaka 5	Taasisi inayohusika
Idadi ya BMUs zilizo anzishwa							Idara ya Uvuvi/Hal-mashauri za Wilaya/ WWF/BMUs
Idadi ya BMUs zilizopata vyeti vya usajili							Idara ya Uvuvi/Hal-mashauri za wilaya/ BMUs
Idadi ya BMUs zinazow-ajibika							Idara ya Uvuvi/Hal-mashauri za wilaya/ WWF/BMUs
Aina ya makosa yanayo-fanyika kwenye raslimali za pwani na bahari							Idara ya Uvuvi/Idara ya Misitu na Nyuki/Hal-mashauri za wilaya/ WWF/BMUs

VIASHIRIA VYA MATOKEO YA KAZI ZILIZOFANYIKA (*OUTCOME INDICATORS*)

Kiashiria	Taarifa za awali	Mwaka 1	Mwaka 2	Mwaka 3	Mwaka 4	Mwaka 5	Taasisi inayohusika
Idadi ya doria zilizo-fanyika chini ya BMUs							Idara ya Uvuvi/Idara ya Misitu na Nyuki/Hal-mashauri za wilaya/ WWF/BMUs
Idadi ya zana har-amu zili-zokamat-wa							Idara ya Uvuvi/Idara ya Misitu na Nyuki/Hal-mashauri za wilaya/ WWF/BMUs
Idadi ya watuhu-miwa walio-fikishwa mahaka-mani							Mhakama Jeshila Polisi Idara ya Uvuvi/Idara ya Misitu na Nyuki/Hal-mashauri za wilaya/ WWF/BMUs
Idadi ya kesi zilizo-tolewa hukumu mahaka-mani							Mhakama Jeshi la Polisi Idara ya Uvuvi/Idara ya Misitu na Nyuki/Hal-mashauri za wilaya/ WWF/BMUs

VIASHIRIA VYA MAFANIKIO YA KAZI ZILIZOFANYIKA *(IMPACT INDICATORS)*

Kiashiria	Taarifa za awali	Mwaka 1	Mwaka 2	Mwaka 3	Mwaka 4	Mwaka 5	Taasisi inayohusika
Idadi ya aina za samaki wanaovuliwa							Idara ya Uvuvi/Halmashauri za wilaya/WWF/BMUs
Uzito wa samaki waliovuliwa kwa aina ya samaki							Idara ya Uvuvi/Halmashauri za wilaya/WWF/BMUs
Mapato ya kaya							Idara ya Uvuvi/Halmashauri za wilaya/WWF/BMUs
Mapato ya BMUs yanayotokana na vyanzo mbalimbali vya mapato							Idara ya Uvuvi/Idara ya Misitu na Nyuki/Halmashauri za wilaya/WWF/BMUs
Idadi/thamani ya mali iliyopo kutokana na uzalishaji mali wa BMUs							Idara ya Uvuvi/Idara ya Misitu na Nyuki/Halmashauri za wilaya/WWF/BMUs

KIAMBATANISHO NAMBA 1

FOMU NAMBA 1 ITAJAZWA NA KATIBU WA BMU WA KIJIJI KILA MWANZONI MWA MWAKA (JANUARI)

UTEKELEZAJI WA SHERIA YA UVUVI

FOMU YA MAELEZO YA MVUVI

MKOA:..... WILAYA:.....

TARAFA.....KATA:.....

KIJIJI:.....

FORODHA.....

TAREHE.....

NA	JINA LA MVUVI	NA. YA UANDIK-ISHWAJI YA BOTI	NAMBA YA CHETI CHA BOTI CHA UN-DIKISH-WAJI NA TAREHE	NAMBA YA LESE-NI YA BOTI NA TAREHE	NAMBA YA LESE-NI YA UVUVI NA TAREHE	ZANA ZA UVUVI, AINA , IDADI NA UKUBWA WA MACHO WA NYAVU & UKUBWA WA /NDOANO	MAONI

KIAMBATANISHO NAMBA 2

MATUKIO YA UVUNJAJI WA SHERIA YA UVUVI, KANUNI ZAKE NA SHERIA NGOGO NDOGO ZA BMU

KUMBUKUMBU ZA KILA SIKU

FOMU NAMBA 2A ITAJAZWA NA KATIBU WA BMU WA KIJIJI

NA	TAREHE	JINA LA MTUHUMIWA	KOSA	HATUA ZILI-YOCHUKU-LIWA	SAHIHI YA MTUHU-MIWA	SAHIHI YA KIONGOZI WA KAZI

KIAMBATANISHO NAMBA 3

MATUKIO MENGINE

FOMU NAMBA 2B ITAJAZWA NA KATIBU WA BMU WA KIJIJI

KUMBUKUMBU ZA KIlA SIKU

NA	TAREHE	TUKIO	TATIZO LILILOJI-TOKEZA	HATUA ILI-YOCHUKU-LIWA	MAONI	MAJINA YA BMUs WALI-OSHUHU-DIA	SAHIHI YA KIONGOZI WA BMU ALIYE-SHUHU-DIA

KIAMBATANISHO NAMBA 4

MUHTASARI WA TAARIFA KWENYE DAFTARI LA KUWEKA KUMBUKUMBU

FOMU NAMBA. 3 ITAJAZWA NA AFISA UVUVI KATA/ TARAFA/WILAYA

NA	TAREHE	KATA	KIJIJI	FORODHA	KOSA/ TUKIO	HATUA ILIYO-CHUKULIWA	MAONI

KIAMBATANISHO NAMBA 5

FOMU NAMBA 4

FOMU YA USHAURI KWA BMUs ITAJAZWA NA MTAALAM/AFISA ALIYETEMBELEA BMU KIJIJINI

TAREHE	JINA	TAASISI	USHAURI WA KITAALAMU ULIOTOLEWA	SAHIHI YA MTAALAM/ AFISA

KIAMBATANISHO NAMBA 6

VYANZO VYA MAPATO KWA BMUs

Wajumbe wa BMUs wataendesha kazi zao kwa kujitolea kwa kuwa wao ndio wanaomiliki na kunufaika na raslimali za bahari na pwani. Aidha, wanaweza kupata mapato na kunufaika nayo kutokana na shughuli mbalimbali ambazo ni zaidi ya hizi zifuatazo:

a) Kuanzisha vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa (Savings and Credit Co-operative Society (SACCOS). Pia, wanaweza kuwa na Akaunti Benki zinazozalisha faida
b) Kuomba uwakala wa kukusanya mapato ya Halmashauri za wilaya
c) Kuanzisha vyama vya ushirika vya kununua na kuuza samaki
d) Kuanzisha miradi mbadala ya kujiongezea kipato kama vile migahawa, maduka, ufugaji samaki, kunenepesha kaa, kilimo cha mwani, kilimo cha mboga mboga, vitalu vya mti, kufuga nyuki, nk
e) Kuanzisha utaratibu wa kutoza ushuru wa kuegesha magari ya mizigo, boti za uvuvi, uchukuzi wa abiria, samaki na mizigo mingine katika forodha/bandari yao
f) Ujenzi wa nyumba za wageni, vyumba vya mikutano, migahawa, stoo, nk
g) Kukusanya michango kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kutunza raslimali za bahari na pwani na
h) Mapato yanayotokana na faini za sheria ndogo ndogo za BMU

KIAMBATANISHO NAMBA 7

MATUMIZI YA MAPATO YA BMUs

Fedha zinazotokana na vyanzo halali vya kazi na biashara ni lazima zitumike kwa njia ambayo itasaidia kuendeleza usimamizi endelevu wa raslimali za bahari na pwani. Pia, ni lazima matumizi yake yawanufaishe wajumbe/wanachama wote wa BMUs na jamii ya wavuvi kwa ujumla.

Kwa hivyo inashauriwa kuwa fedha za BMUs zitumike katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:

a) Kuendesha doria na kuokoa maisha ya watu baharini
b) Kuwekeza katika miradi ya kiuchumi ambayo itasaidia kuongeza mapato yao
c) Kusaidia ujenzi wa huduma za jamii kama vile vyumba vya madarasa, zahanati, nyumba za waalimu, visima vifupi vya maji ya kunywa, barabara za vijijini nk
d) Kupata hati miliki ya maeneo karibu na forodha kwa ajili ya kujenga maeneo ya kupumzika wananchi na vitega uchumi
e) Kuandaa utaratibu wa kutoa mikopo ya riba nafuu kwa ajili ya wanachama wa BMUs
f) Kuchangia katika mafunzo ya muda mfupi ya wanachama wa BMUs katika maeneo ya uongozi, namna ya kutatua migogoro katika jamii, ujasiriamali, usimamizi wa fedha, uwekaji kumbukumbu za fedha, utunzaji was too, utunzaji, usimamizi na matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi/bahari na pwani
g) Kuendesha kampeni za kuimarisha usimamizi shirikishi wa raslimali za bahari na pwani na kuinua uwelewa wa jamii za wavuvi katika kulinda, kusimamia, kuendeleza na kuvuna kwa njia endelevu raslimali na mazingira ya bahari na pwani.

LVEMP (2005) Guidelines for Establishing Community Based Fisheries Collaborative Management in Tanzania.

LVEMP (2005) Operational Manual for Community Based Fisheries Collaborative Management (Co-management) in Tanzania. (English and Kiswahili version).

LVFO (2005) The State of the Fisheries Resource of Lake Victoria and their Management: Proceedings of the Entebbe Regional Stakeholders` Conference. 24-25 February 2005, Entebbe Uganda

LVFO (2007) Guidelines for Beach Management Units (BMUs) on Lake Victoria. LVFO, Jinja.

MNRT (2003) The Fisheries Act, No. 22 of 2003

MNRT (1997) National Fisheries Sector Policy and Strategy Statement

RUMAKI (2004) Programme Document for Rufiji, Mafia and Kilwa districts Seascape

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa (2001) Mafunzo ya Viongozi katika Ngazi ya Kijiji, Mtaa na Kitongoji

URT (2005) Project Implementation Manual for Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP)

Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi

Lengo kuu la Sera ya Taifa ya Uvuvi, ni kukuza uhifadhi, maendeleo na usimamizi endelevu wa raslimali za uvuvi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Sekta binafsi, jamii na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali pamoja na wadau wengine, wana mchango mkubwa katika kutunza, kusimamia, kuendeleza na kudumisha matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi. Hii ni kwa sababu wadau wote hawa wana uzoefu, utaalamu na uwezo tofauti katika nyanja muhimu za usimamizi wa raslimali hizi. Kwa maana hiyo kunahitajika ushirikiano wa karibu baina ya wadau wote ili kuhakikisha kuwa mazingira na raslimali za uvuvi zinabaki kwa faida ya jamii. Usimamizi shirkishi wa raslimali za uvuvi kupitia vyombo vya kijamii kama BMU, unaipa jamii haki na wajibu wa kusimamia na kuendeleza raslimali zilizopo kwa faida ya wote. Hivyo jamii inawajibika kuhakikisha kuwa raslimali zilizopo zinalindwa, zinatunzwa na kuthaminiwa na wao wenyewe kwani ndio msingi wa maisha yao, jamii nzima na taifa kwa ujumla.

WWF

for a living planet®